

## Kushirikiana katika elimu ya mtoto wako

Kwa kuwa mshirika mzuri katika elimu ya mtoto wako, utasaidia kumwandaa mtoto wako kwa mafanikio shuleni na maishani. Tunatarajia kuwa utaendelea kuzungumza na kusoma na mtoto wako kwa lugha yako ya asili nyumbani. Kuzungumza lugha yako ya asili nyumbani kutampa mtoto wako msingi wa kujifunza shuleni, na vijana ambao wanahitimu kuzungumza lugha mbili au zaidi wanapata fursa zaidi za kazi baada ya kuhitimu.



### Maelezo zaidi

Ikiwa unahitaji maelezo zaidi kuhusu mipango ya MLE inayopatikana katika shule yako, wahudumu kwenye afisi ya shule wako tayari kujibu maswali yako.

Ikiwa una maswali ya ziada au unahitaji maelezo zaidi kuhusu kuchagua mpango sahihi wa MLE kwa ajili ya mwanafunzi wako, piga simu 720-423-2040. Wafanyakazi wetu wanaozungumza lugha mbili wanapatikana ili kukupa majibu.

*Video ya Chaguo za Wazazi wa MLE:*

<https://bit.ly/2BnoCzB>

*Namba ya Dharura ya MLE*

**720-423-2040**

*Tovuti*

**[mle.dpsk12.org](http://mle.dpsk12.org)**

Swahili

## MIPANGO YA MLE KATIKA DPS

*Kwa ajili ya wanafunzi wanaojifunza  
Kiingereza*





## Karibu kwenye DPS

Hapa DPS, misingi mingi tofauti ya isimu na tamaduni ambayo wanafunzi wetu wanaleta darasani hutajirisha shule zetu. Ni rasilimali ambayo zikijumuishwa na stadi za lugha ya Kiingereza, huwasaidia wanafunzi kufanikiwa katika shule na maisha. Mipango yetu ya Multilingual Education (Elimu ya Lugha Nyingi)—au MLE—imeundwa mahususi kumsaidia mtoto wako kujifunza Kiingereza wakati mmoja na ule wa kujifunza masomo kama vile kusoma, hisabati na sayansi.

Programu za MLE za DPS zimewasaidia maelfu ya wanafunzi kufanikiwa shuleni na kuhitimu tayari kujiunga na chuo au kazi - wanafunzi wanaobaki katika programu ya MLE hadi wanapokuwa tayari kuhamia darasa la kawaida wana viwango vya juu vya kuhitimu kuliko wanafunzi ambao hawajawahi kuwa katika programu ya MLE.

### Programu za MLE ni nini?

Shule za DPS zina aina mbili za programu za MLE, lugha mbili na Kiingereza kama Lugha ya Pili. Programu za lugha mbili za DPS zimeundwa kwa wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni Kihispania, na zinatoa mafundisho kwa lugha ya Kihispania na Kiingereza. Programu hizo mbili katika DPS ni TNLI (Mafunzo ya Kimataifa ya Lugha ya Asili) na Lugha Mbili/Inayotumia Lugha Mbili kwa Pamoja.

Programu za Kiingereza kama Lugha ya Pili zinapendekezwa kwa wanafunzi wanaozungumza lugha zingine isipokuwa Kihispania. Kama mzazi, unachagua huduma za programu ya MLE ukitumia Fomu ya Idhini ya Mzazi ambayo utapewa wakati wa usajili. Ikiwa huduma za MLE hazipatikani shuleni, mtoto wako anaweza kuhudhuria shule ya MLE la Eneo. Ofisi yako ya shule inaweza kutoa maelezo zaidi kuhusu shule za Eneo la MLE.

### Kingereza kama Lugha ya Pili

Katika programu ya Kiingereza kama Lugha ya Pili (ESL, pia inaitwa ELA-E), madarasa yote ya mtoto wako yatafundishwa kwa Kiingereza. Waalimu katika programu hii wamepewa mafunzo maalum ili kuwasaidia wanafunzi kujifunza Kiingereza wanapoendelea kujifunza masomo mengine kama vile kusoma, sayansi na hisabati. Shule yako inaweza pia kutoa usaidizi wa ziada katika lugha yako kupitia mwalimu wa lugha ya asili.

Aidha, mtoto wako atakuwa na kipindi cha dakika 45 kwa kila siku kilichotengwa kujenga msingi imara wa kujifunza jinsi ya kuzungumza na kuandika kwa Kiingereza, kinachoitwa Kuendeleza Lugha ya Kiingereza.

**Ili kuchagua huduma za Kiingereza kama Lugha ya Pili, chagua CHAGUO LA 2 kwenye Fomu ya Idhini ya Mzazi.**